**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY

**April, 2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

Mkuu wa Shule***-0754 088 341/ 0785 758 063***

Makamu Mkuu wa Shule**-0787 474 402**

Matron/Patron**-0614 870 978**

**Shule ya Sekondari**

**Embarway**

**S.L.P 41 Tarehe 24/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**…………………………………………….. S.L.P ……………………………………..**

**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY HALMASHAURI YA NGORONGORO MKOA ARUSHA MWAKA 2024/2025**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024 kwa tahasusi ya HGL/HKL/HGK/HGE/HGFa/HGLi au CBG.
2. Shule ya Sekondari Embarway ni shule ya bweni na ipo ndani ya mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Tarafa ya Ngorongoro, kata ya Enduleni, Kijiji cha Enduleni.
3. Usafiri wa landrover kutoka mjini Karatu unapatikana katika kituo cha mabasi Karatu Stendi nauli ni shilingi 10,000/= mpaka shuleni.
4. Muhula wa Masomo unaanza tarehe ........... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............na mwisho wa kuripoti ni tarehe .........

## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

1. Sare ya shule ni sketi 2 rangi ya Mkidoma (crystal teal green), angalia picha mwishoni mwa fomu hii
2. Shati mbili nyeupe mikono mirefu (aje nazo)
3. Tai 2 zenye mistari ya dark blue
4. Rangi ya hijab (kijuba) ni nyeupe ndefu (kwa wanafunzi waislamu, aje nazo)
5. T- shirt 02 za darasani zenye kola (form six)
6. Sare ya michezo kwa shule ni
    a. Raba nyeupe jozi 01
    b. Socks nyeupe ndefu za michezo pair 2
    c. Jezi ya michezo pea 01 (T-Shirt iliyoandikwa Tanzania kifuani) rangi nyeupe
    d. Tracksut.
7. Viatu vya shule ni vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi
8. Soksi jozi mbili nyeupe za shule (stocking)
9. Sweta 02 lightblue
10. Nguo za kushindia gauni (shamba dress) 02 rangi ya damu ya mzee (aje akiwa amevaa), angalia picha chini

### 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

A. Mwanafunzi anapaswa kuja na

I. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka
II. Scientific calculator kwa wanafunzi wote isipokuwa atakayekuwa anasoma tahasusi ya HKL
III. Apron nyeupe kwa wanafunzi wa CBG kwaajili ya mazoezi kwa vitendo (practicals)
IV. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology
V. Godoro 01 (size) 3”x 6ft x 3ft (tanform/Super Banco)
VI. Mashuka pair 02 pinki ,blanketi 01, Taulo 01, chandarua 01, nguo za ndani kumi kila mmoja
VII. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe visiwe vya plastic)
VIII. Ndoo moja ya lita 10 yenye mfuniko –
IX. Ruber squeezer 01, Hardbroom 01 na jembe 01 kwaajili ya usafi (vifaa hivyo atatumia yeye mwenyewe)
X. Kumbuka kuja na kopi moja ya result slip na cheti cha Kuzaliwa.

### 1.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango ilipwe kwenye account ya shule**

BANK**: NMB**
JINA **: EMBARWAY SEKONDARI**
ACCOUNT**: 40901000004**

2. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule pamoja na makosa yatakayosababisha mtoto kufukuzwa shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**2.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2** Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**A.** UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI

Mimi kwa hiari yangu ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha tano 2024/2025 katika Shule ya Sekondari Embarway.

- Nitakuwa tayari kuzifuata sheria za shule kama zilivyoandikwa hapo juu, aidha nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kusimamishwa masomo endapo nitatenda makosa yaliyoainishwa hapo juu,
- Nitahudhuria masomo yote kila siku; na kufanya mazoezi, majaribio yote na mitihani yote kikamilifu.
- Sitashiriki katika hila zozote za wizi au udanganyifu wa mitihani,
- Nitashiriki katika klabu za kimasomo na michezo mbalimbali shuleni na wala sitaacha shule kamwe bila taarifa.
- Nitahudhuria maandalio (preparation) yote ya mchana na usiku ili kujisomea na si vinginevyo.
- Nifukuzwe shule mara moja endapo nitaonekana nazurura mitaani, porini (wakati wowote) au bwenini wakati wa vipindi.
- Ninaahidi kusoma kwa bidii na kuwatumia walimu wangu vizuri kitaaluma na nitatii mashauri yote yanayotolewa na wazazi/walezi na walimu wangu siku zote.

……………………………… …………………
Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

## HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili (majina matatu)
2. Tarehe ya kuzaliwa (kama ilivyo kwenye cheti)
3. Dini ………………………………………… dhehebu …………………………………..
4. Mahali na wilaya alipozaliwa ……………………………………………
5. Shule ya sekondari alikohitimu kidato cha nne……………………………..
6. Mambo anayopendelea kufanya nje ya masomo

a) ………………………………b)............................... c)......................................

.

**NB: Muhimu**

**Njoo na Fomu zote zikiwa zimejazwa vizuri na kutiwa saini na wahusika wote kwani fomu hizo zitatumika kufungua jalada la mwanafunzi.**

.........................................................

**FIDELIS E.BILALY**

HEADMASTER
EMBARWAY SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 41 NGORONGORO
DATE ______________

**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NGORONGORO DISTRICT COUNCIL EMBARWAY SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**To be completed by Medical officer only**

**Name of student ……………………………………..…………………..Age……………………….……………………**

1. HIV test ………………………………………………………………………………
2. Blood count (White & red)…………………………………………………………
3. Urine examination …………………………………………………………………
4. UTP (For female)
5. Stool examination …………………………………………………………………
6. Syphilis test …………………………………………………………………………
7. TB test ………………………………………………………………………………
8. Ear test ………………………………………………………………………………
9. Eye test ………………………………………………………………………………
10. Abdomen ……………………………………………………………………………
11. Spleen ………………………………………………………………………………
12. Additional information or any other physical, mental hereditary or infections diseases ……………………………………………………………………………………………….. (please state nature of treatment)

**Medical certificate**

**I certify that the above mentioned student has been examined and found him/her to be fit/unfit to pursue further education.(delete whichever not needed)**

**Name …………………………………… signature ………………………………………**

**Designation …………………………… station ……………………………………………**

**Date ……………………………………**

**Official stamp**

**MFANO WA SARE ZA SHULE (MASHONO NA RANGI)**





**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOANDIKWA HAPO JUU**

**3. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**